**TAARIFA FUPI YA TOVUTI WAKATI WA UZINDUZI WA TOVUTI MPYA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) SIKU YA IJUMAA MEI 27, 2022 JIJINI DODOMA KATIKA UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE CONVENTION.**

## 1. UTANGULIZI

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni moja ya taasisi ambayo ilikuwa inatumia tovuti iliyotengenezwa mwaka 2017 kwa msaada wa mfadhili kupitia mradi wa kutengeneza tovuti katika Ofisi za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hapa nchini mara baada ya kuanzishwa kwake. Tangu kipindi hicho hadi kufikia **Mei 17, 2022** tovuti hiyo ilitembelewa na wadau mbalimbali wapatao **182,650** pamoja na changamoto kadhaa zilizokua zinajitokeza katika usimamizi wake kwa kadri ilivyokua inatumika na kwa kiasi kikubwa changamoto hizo zilikuwa zinaathiri ufanisi wake kutokana na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia duniani katika eneo la habari, elimu, mawasiliano na uhamasishaji kwa njia na zana zote za mawasiliano ya kimkakati. Baadhi ya changamoto zilizoainishwa ni:-

i. Tovuti kutengenezwa kwa teknolojia ya zamani;
ii. Waendeshaji tovuti kutokuwa na uelewa wa kutosha kwenye masuala ya usimamizi wa tovuti hiyo;
iii. Uhitaji mkubwa wa kuboresha mwonekano na maudhui ya tovuti;
iv. Uelewa hafifu na fasaha wa namna ya kuandaa na kupandisha taarifa, takwimu na nyaraka mbalimbali kwenye tovuti;
v. Maafisa TEHAMA, Habari na Mawasiliano ya Serikali kutokuwa na umiliki wa moja kwa moja (ownership) hali ambayo imesababisha changamoto katika kuhuisha taarifa na kufanya maboresho mbalimbali kwa wakati; na
vi. Tovuti kutokidhi mahitaji ya Tume kwa kutokuwa na maeneo ya kutosha kwa ajili ya kuweka taarifa mbalimbali za Taasisi.

Kutokana na kuwepo kwa changamoto hizo, Tume iliamua na kuelekeza kupitia Kamati ya TEHAMA kujadili utekelezaji wa suala hilo na

kutengeneza tovuti mpya itakayoleta suluhisho la changamoto zilizoainishwa na ambayo itakidhi vigezo vyote vinavyohitajika.

## 2. MATENGENEZO YA TOVUTI MPYA

Zoezi la kutengeneza tovuti lilianza baada ya maelekezo ya Tume kwa Menejimenti kupitia Kitengo cha TEHAMA, Mawasiliano ya Serikali, Manunuzi, Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu pamoja na Wataalam wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP), kubainisha mahitaji ya Tume (identify requirements).

Baada ya kukamilisha hatua hiyo, e-GA walipewa jukumu la kutengeneza tovuti hiyo mwaka 2020 na walifanya kazi hiyo kwa kuanza na hatua ya usanifu (designing) na baadae kuunda tovuti (development) huku wakishirikisha maafisa wa TSC (TEHAMA na Mawasiliano ya Serikali) kwa kila hatua ambapo mara kadhaa kulikuwa na majadiliano ili kukubaliana namna bora ya kufanya.

Tovuti mpya ilikamilika mwezi Januari, 2022 ambapo gharama zilizotumika kutengeneza tovuti hiyo ni **Shilingi Milioni Sita (Tzs.6,000,000/=).**

Baada ya kukamilika kwa tovuti hiyo, Maafisa wa TSC (TEHAMA na Mawasiliano ya Serikali) walipatiwa mafunzo ya namna ya kusimamia na kuhuisha taarifa mbalimbali kwenye tovuti hiyo. Mafunzo hayo yalifanyika mwanzoni mwa mwezi Aprili, 2022 jijini Dodoma na yamefanya maafisa kuweza kuisimamia tovuti hii na kupandisha taarifa mbalimbali ambapo hadi sasa asilimia 90 ya taarifa zinazohitajika zimepandishwa. Matumizi rasmi ya tovuti hii mpya yataanza mara baada ya uzinduzi hii leo kwa kuitoa hewani ile ya zamani na kuipandisha hewani hii mpya.

## 3. FAIDA ZA TOVUTI MPYA

Tofauti na tovuti ya zamani, tovuti hii mpya ni bora zaidi kwa kuwa: -

a) Tovuti ya sasa inakidhi mahitaji ya Tume kutokana na uwezo wake wa kubeba taarifa nyingi zaidi kwa wakati mmoja;
b) Tovuti hii inaendana na Teknolojia ya kisasa;
c) Tovuti mpya ina uwezo mkubwa wa kuingiza na kupokea maudhui na maboresho ya taarifa kwa wakati;
d) Maafisa wa TSC (TEHAMA na Mawasiliano ya Serikali) wana uelewa wa kutosha katika usimamizi (administration) na uendeshaji wa tovuti hii; na
e) Tovuti hii inamsaidia mtumiaji (Walimu wanaohudumiwa na Tume wapatao **258,291 (Msingi 173,591 na Sekondari 84,700)** na wadau wengine wa Tume) kupata viunganishi (link) vya Mifumo mbalimbali kwa urahisi.

Aidha, pamoja na faida hizo huduma na vitu vitakavyopatikana katika tovuti hii mpya ni pamoja na; Ufahamu wa Majukumu ya Tume kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Tume, Sheria ya Tume na Kanuni zake, maelezo na taratibu za upatikanaji wa huduma mbalimbali zitolewazo na Tume, machapisho mbalimbali ikiwemo Miongozo, Mipango Mkakati, Tafiti, Taarifa, Sera, Majarida, Takwimu, Fomu mbalimbali za mtandaoni katika Utumishi wa Umma, na eneo la habari ambamo kutakua na Taarifa mbalimbali kwa Vyombo vya Habari, Hotuba, Vipeperushi, Vibango, Vibonzo, habari picha mnato, habari picha jongefu, Mawasiliano ya Tume pamoja na ramani mtandao ya kufika Ofisi za Tume Makao Makuu, Dodoma na Ofisi za Wilayani zote 139.

## 4. SHUKRANI NA PONGEZI

Tunapenda kutoa shukrani za pekee kwa Mwenyekiti wa Tume na Makamishna kwa ujumla kwa kuona umuhimu wa kuwa na tovuti iliyo bora, inayokidhi vigezo na miongozo ya Serikali, iliyo hai na bora kiteknolojia kwani mara kwa mara walikuwa wakiielekeza Menejimenti kuwa na tovuti inayokidhi mahitaji ya Tume na wadau wake.

Pia Kitengo cha TEHAMA na Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali tunapenda kumshukuru Mtendaji Mkuu (Katibu wa Tume) na Menejimenti kwa ujumla kwa kukubali na kutuwezesha kuifanya kazi hii kwa ufanisi.

Hali kadhalika, tunaishukuru Mamlaka ya Selikali Mtandao (e-GA) kwa ushauri na kazi kubwa ya kutengeneza tovuti hii, Kamati ya TEHAMA ya Tume kwa maoni na ushauri wao, Idara na Vitengo vyote kwa kuandaa maudhui na taarifa mbalimbali ambazo zitatumika kwenye tovuti hii pamoja na Kitengo cha TEHAMA na Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kwa kuratibu zoezi la matengenezo ya tovuti hii bila kuwasahau wengine wote walioshiriki kufanikisha kazi hii.

## 5. HITIMISHO

Ni matarajio yetu kuwa tovuti mpya iliyoboreshwa itakuwa ni chanzo sahihi na bora cha taarifa mbalimbali kuhusu Tume kwa Walimu, Wananchi, Wadau wa Elimu na Taasisi mbalimbali. Taarifa na Maudhui yaliyopo kwenye tovuti yatatumika katika kazi mbalimbali ikiwemo kujifunza, kufanya tafiti, kupata huduma na rejea ya nyaraka mbalimbali kuhusu masuala ya Utumishi wa Walimu. Aidha, Kitengo cha TEHAMA kimejipanga kusimamia tovuti hii kikamilifu ili iweze kufanya kazi na kupatikana kwa muda wote. Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali nacho kipo tayari kuhuisha taarifa kwa kadri zinavyohitajika ili wadau wetu waweze kupata taarifa kwa wakati na waweze kutumia huduma zilizopo kwenye tovuti hii.

**Imewasilishwa na:**

CHAMI, Gerard Julius
**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa